

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA  
SHULE YA SEKONDARI IKIMBA  
S. L. P 261, KYELA**

.....

Kumb. Na. IKB/FI/S/VOL 1/2021

MWANAFUNZI: .....

KYELA

**MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninayofuraha kukutaarifu kuwa, umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka 2021, hongera sana. Shule ya sekondari Ikimba iko umbali wa km 16 Magharibi mwa mji wa Kyela. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/1/2021 unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/1/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/1/2021. Unatakiwa kufika bila kukosa.

**2.0 MAHITAJI MUHIMU**

**2.1 SARE YA SHULE**

**A. Wasichana**

- ▶ Sketi mbili ndefu za rinda box (Marinda sita-6)  
(Rangi ya ugoro iliyokolea na kijani jeshi)
- ▶ Mashati mawili meupe mikono mifupi.
- ▶ Soksi ndefu nyeupe jozi mbili
- ▶ Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba visigino vifupi.
- ▶ Kwa Waislamu rangi ya Hijabu ifanane na rangi ya sketi.
- ▶ Track suit rangi ya dark blue jozi moja
- ▶ Raba za michezo

**B. Wavulana**

- ▶ Suruali ndefu za heshima zenye marinda, zilizopindwa chini (Turn up). Rangi ya Ugoro iliyokolea na Kijani jeshi. Suruali za kubana kama vile vichupa, vinjiwa na modo haziruhusiwi.
- ▶ Mashati mawili meupe mikono mifupi.
- ▶ Soksi nyeusi jozi mbili.
- ▶ Mkanda mweusi wenye chuma cha kawaida cha heshima.
- ▶ Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba visigino vya kawaida.
- ▶ Track suit rangi ya dark blue jozi moja
- ▶ Raba za michezo

**NB: Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa viatu vya plastiki kama vile Yeboyebo, Bajaji n.k**

## 2.2 MAHITAJI MENGINE

- Bunda la karatasi (Ream) kwa ajili ya mazoezi na Majaribio.
- Daftari 11 (Counter Book Q2)
- Kalamu za wino (bic) na kalamu za risasi (penseli)
- Mkebe mmoja na rula
- Ni wajibu wa Mzazi kumpatia Mwanafunzi nauli ya kuja na kurudi shuleni, Chakula cha mchana, gharama za matibabu na kuhudhuria vikao vyote shuleni bila kukosa.
- Ndoo ya lita kumi (10) kwa ajili ya usafi

## 2.3 MAMBO MENGINE MUHIMU YA UNAYOPASWA KUKAMILISHA NA KUWASILISHA SHULENI WAKATI WA KURIPOTI

- a) Fomu ya hospitali (Medical examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu inapatikana shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi na Mkatiba wa kutoshiriki katika Migomo, Fujo na Makosa ya jinai.
- c) Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa shuleni.

## **TAFADHARI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/ MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU KABLA YA KUJA SHULENI**

***“KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI IKIMBA”***

---

**ROBERT T MWAKAFWILA  
MKUU WA SHULE  
0766738615 AU 0620400987**